Vyombo Vya Muziki (Instrumental Music)

Na

J. D. Logan

Vyombo Vya Muziki

Na

J. D. Logan

Novemba 5, 2011

Vyombo Vya Muziki

Utambulisho

Wakristo wameagizwa kumwimbia Mungu katika ibada. Hii haijawahi kubishwa. Hata hivyo, kuna ubishi unaoendelea kwamba vyombo vya muziki zilizotengenezwa zinaweza kutumika katika kusaidiana na nyimbo wakati wa kuimba. Kusudi la uchunguzi huu ni kuuangalia mkanganyiko huu katika maandiko na misimamo ya kihistoria.

Misimamo miwili hii ni katika maandiko. Hataivyo, kihistoria inaweza kutoa mwanga katika mafundisho ya awali na matendo ya awali ya kanisa ya mitume. Hili ni muhimu kufahamu, kama matendo mengi na mafundisho yameongezwa katika yale yaliohalisi ya kanisa kama ilivyoanzishwa na mitume.

Kihistoria Kabla ya 300 AD

Aquinas. "Kanisa letu halitumii vyombo vya muziki, kama filimbi na kinanda, kumsifu Mungu na vyote, ili asiweze kuonekana Myahudi." (Thomas Aquinas, Zama za kale za Bingham, Tol. 3, Ukurasa 137).

Agustino. "Vyombo vya miziki zilikuwa hazitumiki. Bomba, kinanda, na filimbi hata vinahusiana na kusisimua wale wasioamini, vile vile na matendo ya ajabu na michezo ya haibu katika kumbi za vizazi na uovu. Ni rahisi kufahamu majivuno yao dhidi ya matumizi katika ibada." (Agustino, 354 AD, inaelezea uimbaji huko Alexandria chini ya Athanasius).

Hii itatumika katika kuonyesha matendo na mafundisho ya kanisa la kmitume la ghafla. Sitanukuu zingine, bali nitataja baadhi ya majina machache ambayo malengo yao huonyesha nia iyo hiyo. Miongoni mwa wengine kuna, **Chrysostom,** (381 – 407), **Clement wa Alexandria,** (190 AD Mwalimu, baba wa kanisa, Uk, 130; **Erasmus,** (Komentari ya Erasmus katika 1 Kor. 14:19); na **Eusebius**, (Komentari katika Zaburi 91:2-3).

Katika muingiliano wa karne hadi katika miaka ya "Urejesho" (Calvin Luther, Wesley) kanisa la Roman Katholiki lote lilianzisha kinanda. Ilisemekana Papa Vitalian kuwa wa kwanza kuanzisha kinanda katika kanisa. Hii ilikuwa katika mwaka 666. Kulikuwa na pingamizi nyingi katika makanisa ya Magharibi mwa Uropa kwa sababu ya nyongeza ya kinanda. Hakukuwa na makubaliano ya pamoja ya matumizi haya ya vyombo hadi baada ya karne ya nane.

Kwamba kanisa la Warumi kuwa la kwanza kuanzisha tendo hili halishangazi, kwa mtazamo wa matendo ya Wapagani alioanzisha katika muongo huu. Cha kushangaza, hili linakubaliwa na baadhi ya wanahistoria wake wenyewe, kama tunavyoweza kuona ifuatavyo: "Tunapaswa kuwa wazi katika kukubali kwamba mishumaa, kama dhabihu na maji yenye rangi, vilitumika sana katika ibada za wapagani haki inayolipwa kawa wafu. Lakini Kanisa, katika wakati wa awali, ilizichukua na kuziingiza katika matumizi yake, sawa na jinsi mwanamke huyu alivyoanzisha vitu vingi zilizotofauti zenyewe kwa zenyewe, iliyooneka vyema kurithi mwongozo wa sherehe za kidini. Lazima tusisahau kwamba nyingi ya hizi vifaa (nyongeza…JDL) kuabudu, kama mwanga, **muziki**, (vyombo…JDL) marashi, mapambo, michoro ya sakafuni, mapambo ya sehemu ya mbele ya nyumba, vioo, kengele, chakacha, nk. Haikuwahi kutambulika na jamii ya waabudu sanamu lakini zilikuwa maarufu karibia katika jamii zote." (Kamusi kubwa ya Wakatholiki, Tol. 3, Uk. 246).

Wakati wa "Marekebisho"

Katika wakati wa "Marekebisho", viongozi wa mchakato huu (katika Uropa Magharibi) walikataa matumizi ya vyombo vya ibada. Miongoni mwa mafundisho hayo dhidi ya hili, tukitaja wachache walikuwa ni **Calvin**, muanzilishi wa kanisa la Presbyterian; **Wesley,** mwanzilishi wa Kanisa la Methodist; **Luther**, muanzilishi wa Kanisa la Kilutheri; **Spurgeon**, mmoja wa wakuu wa Kanisa la Kisabato ambaye hajawahi kuishi.

Wesley aliandika, "Sina pingamizi katika vyombo vya muziki katika ibada yetu, ikiwa zinaonwa au kusikilizwa." (Kutoka katika Komentari ya Adam Clarke, Tol. 4, Uk 685).

Luther aliandika, "Chombo katika ibada ni alama za cheo cha Baal… Roman Katholiki waliiazima kutoka kwa Wayahudi." (Encyclopedia ya Martin Luther, McClintock & Strong's, Tol. 6, Uk 762). (Je, hatupaswi kurudisha kila kitu tulichoazima? JDL).

Hii ni kutaja vichache, lakini kimsingi kulikuwa na wengine wadogo miongoni mwa hao "Warekebishao" waliofundisha kinyume na tendo hili.

Imekuwa tu katika miaka ya hivi karibuni kwamba vyombo vya muziki zimetapakaa sana kwamba watu wema wengi wanashangaa kwamba kuna watu wa dini ambao hawatumii vyombo vya muziki katika ibada zao. Hataivyo, leo, vyombo vya muziki zimekubaliwa (kwa machache ya kipekee) katika ulimwengu wote wa kidini na haihojiwi.

Miongoni mwa Makanisa ya Kristo

Ilikuwa ni 1860 ambapo Lewis L Pinkerton wa Midway, Kentucky kwanza alifanikiwa kuanzisha chombo cha muziki ili kusaidia katika uimbaji wa kusanyiko. Chombo hiki hakikuwa filimbi au kinanda bali sauti tamu. Ilipingwa na makusanyiko mengine miongoni mwa ndugu wote na ilihubiriwa kinyume na wahubiri wengi wa siku hizo, hata kama baadhi waliikubali.

Kufuatia Vita vya Kijaamii, makanisa mengi ya Kaskazini ziliiga matumizi ya vyombo bali wale wa Kusini kwa ujumla wakaikataa. **J W McGarvey,** mmoja wa wahubiri wa nyakati hizi aliyesimama imara aliandika, Hivyo basi, hatuwezi, kwa uwezekano wo wote kufahamu kwamba kifaa cha ibada kinakubaliwa na Mungu katika kizazi cha Kikristo, wakati Maandiko maandiko yanayonena kuhusu kizazi kile ziko kimya kuhusiana na swala hili. Kuanzisha swala kama hilo si kimaandiko na ni makusudi. Ni ibada ya kupenda, ikiwa kitu kama ibada ya kupenda inaweza kuwepo. Kwa sababu hii tunalaani kuchomwa kwa dhabihu, kuwasha mishumaa, kuvaa nguo ndefu za kikuhani, na kusoma vijitabu vya maombi. Katika msingi huo huo tunalaani vyombo vya muziki." (*Millennial Harbinger,* 1864, 511).

Mwingine aliyepinga vyombo alikuwa ni **David Lipscomb.** Huyu mhubiri wa zamani mzuri alipigana kuhusu kuanzishwa huku kwa vyombo vya muziki maisha yake yote. Wahubiri wengi wa kwanza walipinga uanzishwaji wa muziki, lakini ninawanukuu hawa ili kuonyesha ukengeufu wa yale makanisa ya mlengwa wa kushoto wa wakati ule.

Kwa bahati mbaya, makanisa mengi yalikubali vyombo, wakilazimisha swala hili wakati wa mkanganyiko uliofuata, ukisababisha mpasuko mpana miongoni mwa makanisa. Hii iliendelea hadi 1906, wakati serikali ya Marekani katika sensa yake ya dini ilipogundua kile kilichokuwa cha kawaida kwa kila mmoja aliyejali: Makanisa yaliyofanyiwa "Marekebisho" yalikuwa makanisa wawili tofauti, moja kwa moja tofauti. Wale waliokubali vyombo vya muziki walitambulika kwamba ni "Kanisa la Wakristo" na wale waliokataa walitambulika kama "Kanisa la Kristo". Sisemi kwa kumaanisha kwamba mgawanyiko huu ulisababishwa na kuanzishwa kwa vyombo; kulikuwa na mambo ya asili, lakini, kwa somo lililopo, chombo kilikuwa na maana.

Hii ni historia fupi; kuna zaidi, zaidi sana. Hataivyo, mtazamo wa kimaandiko ndio kitu muhimu sasa tunaweza kuangalia hili.

Rekodi Ya Kimaandiko

Orodha ifuatayo inajumlisha kila onyesho katika "muziki" kuhusiana na kanisa la Agano Jipya lililoanzisha na mitume. Ni muhimu kutambua kwamba hii ndio rekodi ambayo Mungu anahitaji watu wake kwa njia ya ibada ya muziki.

- *Nao walipokwisha kuimba wakatoka nje kwenda mlima wa Mizeituni.*" (Mat. 26:30; Mk. 14:26).
- *Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza.*" (Mdo. 16:25).
- *Tena ili mataifa wamtukuze Mungu kwa ajili ya rehema zake; kama ilivyoandikwa, kwa hiyo nitakushukuru kati ya mataifa, nami nitaliimbia jina lako.*" (Rum. 15:9).
- *Imekuwaje basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia.*" (1 Kor. 14:15).
- *Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu.*" (Efe. 5:19).
- *Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.*" (Kol. 3:16).
- *Akisema nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kanisa nitakuimbia sifa.*" (Ebr. 2:12).
- *Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na ombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi.*" (Yak. 5:13).

Hitimisho Lililopatikana Kutoka Katika Maandiko

Hakuna hata takwimu moja inayoelezwa katika kanisa la Agano Jipya lililovuviwa inayoruhusu matumizi ya vyombo vya muziki katika ibada. Uchunguzi wa kina wa Agano Jipya lote hauwezi kutoa neno moja kwa upendeleo.

Kanisa la Kristo ni taasisi ya Agano Jipya. Agano Jipya linafunua kile anachokitaka Mungu, na atalikubali katika kanisa lake. Imewahi kusemwa kwamba Agano Jipya liko kimya

kuhusiana na swala hili la matumizi ya vyombo vya muziki. Ni wazi kwamba wale wanaotumia vyombo vya muziki katika ibada wanafanya hivyo bila kuwa na mamlaka ya kimaandiko.

Kristo alipopaa kwenda mbinguni wakati wa mwisho wa safari zake, Roho Mtakatifu alitumwa ili kuwaongoza mitume katika matendo yote ya ibada yao. Roho aliwaongoza katika uimbaji na kuwaimiza kuimba, lakini sio kupiga vyombo vya muziki katika ibada. Mitume walikuwa waaminifu katika agizo hili.

Kukwepa mafundisho ya wazi ya Agano Jipya, watumiaji wa vyombo vya muziki wamebuni mbinu ambayo mimi naiita **dosari ya kufisha** ili waweze kuthibitisha upotevu huu. **Dosari** hii inatokana na wazo kwamba kama maandiko yamekaa kimya katika kila kitu, tuko katika uhuru wa kuanzisha kile tunachokitaka katika huduma ya Mungu.

Kulingana na mfumo huu wa kufikiria, kama Agano Jipya halisemi, 'Usitumie vyombo' na kwa vile hakuna hukumu ya moja kwa moja ya tendo hili, basi inakubalika kwa Mungu. Wazo hili haliko sahihi, imechukuliwa kama ilivyo kutoka katika upotevu wa watu kwamba ukimya wa neno la Mungu yafaa kama kiongozi katika mfumo huo uo kama ilivyo agizo la moja kwa moja.

Aina ya maagizo

Kuna aina mbili za maagizo katika neno la Mungu; maalum na jumla. Wakati Mungu anapotoa tendo maalum la ibada, hatuachii sisi kuamua.

Zingatia yafuatayo:

Agizo maalum

- Mkate na uzao wa mzabibu vilikuwa vitu maalum katika mez alikuwa maalum kwa familia ya Kiizraeli kama ishara ya sikukuu ya Pasaka. (Kut. 6:14) Nani anaweza kusema kwamba ng'ombe anaweza kukubaliwa?

- Mwana kondoo alikuwa maalum kwa familia ya Kiizraeli kama ishara ya sikukuu ya Pasaka. (Kut. 6:14) Nani anaweza kusema kwamba ng'ombe anaweza kukubaliwa?

- Mungu alimuagiza Nuhu, "*Tengeneza safina ya mti wa mvinje*." (Mwa. 6:14). Je Mungu angependezwa kama Nuhu angetumia mti wa mshita?

Agizo la jumla

- Mungu aliagiza, "*…Nendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe.* (Mk. 16:15). Hakuweka wazi kwamba ni kwa jinsi gani twende, hivyo kwa njia yo yote inakubaliwa. Lakini aliweka wazi cha kuhubiri (injili) na hiyo iliondoa kuhubiri chochote isipokuwa injili.

- Kama Agano Jipya lingesema "Fanyeni muziki", tungekuwa huru kufanya aina yoyote tunayotaka, aidha ya sauti au vyombo; labda vyote kwa pamoja. Hii inaweza kuwa mfano wa agizo la jumla. Lakini agizo ni maalum; imba. Siyo juu yetu kuamua mfumo ambao tunaotii.

Ubishi dhidi ya matumizi ya vyombo

- Neno *psallo* inapatikana mara tano katika Agano Jipya…(Rum. 15:9, 1 Kor. 14:15 [mara mbili], Efe. 5:19 na Yakobo 5:13. Kulingana na kitabu cha Strong, (kumb namba 5567) maana ni "shtusha au shtua i.e kucheza katika chombo cha muziki chenye waya (sherehekea ibada ya kipekee na muziki na vifaa visaidiavyo.)" Neno hili linaruhusu kanisa kutumia vyombo vya muziki katika ibada. (Kutoka katika kitabu kisisimuacho cha Strong)

Jibu

Tafsiri hii ipo tu juju, na inaonyesha upendeleo wa mwandishi. Angalia kitabu cha Vine fafanuzi ya maneno ya Biblia), "kushtusha, shtua, alafu kucheza vyombo ambacho ni cha nyuzi kwa vidole, alafu kwa Upande. (Sheria ya Musa, JDL) kuimba kwa kutumia filimbi, imba zaburi…inachangia katika Agano Jipya kuimba nyimbo za rohoni,kuimba sifa."

Kama ilivyo kwa maneno mengi, maana ya maneno ya sasa yanatolewa katika mizizi ya kale na maneno ya sasa hayafanani na yale ya kwanza. Neno hili limezungushwa na haichukui tena maana halisi.

Kueleza; Neno *psallo* linatafsiriwa imba katika tafsiri 12 katika tafsiri ya kawaida na ya kisasa. Awali, mtafsiri aliamini kwamba neno linamaanisha kuimba au wangeweza kuainisha kuimba kwa vyombo.

Kwa nyongeza, Kanisa la Kiyunani la Kiorthodox hawakuwahi kutumia vyombo katika ibada. Hakika wanapaswa kufahamu maana ya *psallo*, kwa vile ni neno la Kiyunani. Huu ni ushabiriano mzuri ya tafsiri ya kweli ya *psallo.*

***** Vyombo vya muziki zilitumika katika ibada za mahekaluni na makuhani na Walawi.tunaweza kuutumia mfano huu kwa matumizi ya vyombo katika ibada ndani ya kanisa.

Jibu

Ni kweli kwamba kila aina ya vyombo vya muziki zilitumika katika sherehe za hekaluni chini ya Sheria ya Musa. Pia kulikuwa na uvaaji wa mavazi marefu ya kikuhani, kuchezea vyombo, kutoa wanyama dhabihu, nk. Swali siyo kwamba ama vitu hivi vilikuwa au havikuwa sehemu ya ibada hekaluni, bali ni mfano wetu kufuata wakati wa Wakristo. Mwandishi aliyevuviwa wa Agano Jipya alikuwa na cha kusema kuhusiana na hili.

Chini ya Sheria, Wayahudi walikuwa na sherehe zao, pamoja na wanyama kutolewa dhabihu katika mahema walipokuwa katika vyika. Hii ilikuwa chini ya Agano la Kwanza. (angalia Ebr. 9:1). Yaliyojumuishwa katika hema ni mishumaa iliyowashwa, meza, mkate wa wonyesho. Hii ilikuwa ndani ya hekalu iliyotenganishwa na pazia ya Patakatifu pa Patakatifu. Makuhani walitoa huduma kwa Mungu kila siku ndani ya hekalu, lakini Patakatifu Papatakatifu paliingiwa mara moja kwa mwaka na kuhani mkuu pekee. (Ebr. 9:6-7).

Mwandishi wa Waebrania anaonyesha kwamba wakati hema la kwanza (hekalu) iliposimama, ilikuwsa ni kama **umbo** ya njia ya kweli katika takatifu ya yote. (msit. 8) Toleo la zawadi na dhabihu zilikuwa sehemu ya huduma hii. (msit. 9).

Daudi alisema kumsifu Mungu katika hema lake (hema – hekalu) kwa sauti za tarumbeta, kinanda na filimbi. Pia, pamoja na kuchana nguo na kucheza, vyombo vya nyuzi, vyombo vya sauti na vyombo vya sauti za juu. (Zab. 150:1-6).

Yote haya yalifanyika wakati hema la kwanza lilipokuwa linasimama. Mambo haya hayakukusudiwa kuondoa dhambi, au kuwafanya waabudu kuwa wakamilifu, kulingana na dhamira. (Ebr. 9:1-10) zilitumika kama kivuli ya mambo yajayo. (Ebr. 8:9, Kol. 2:17). "*Basi torati kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, **wala si sura yenyewe ya mambo hayo**, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao.* (Ebr. 10:1). Neno kuu hapa ni "*wala si sura yenyewe ya mambo hayo*." Huduma ya hekalu ilikuwa ni kivuli cha mambo mema na makuu yajayo. Hakika, inaweza kuonekana hivyo sisi kama Wakristo, tunaweza **kuiga** huduma halisi za hekalu, tunaweza kujumuisha kuchomwa kwa manukato, kuwatoa wanyama sadaka, sadaka ya kuchomwa, kucheza, pamoja na kuvaa nguo ndefu za makuhani na ukuhani wenyewe bado utakuwa ungali katika nafasi.

Inakubalika tu kuchukua au kuchagua kutoka katika ibada ya Kiyahudi kile tu tunachokitumia, kuacha zingine, au hatupaswi kuridhika na sehemu hiyo ambayo Mungu anatutaka kutunza? Maombi yalikuwa moja ya huduma ya hekalu, pamoja na kuchomwa kwa manukato, dhabihu ya wanyama. Wakristo leo ndio wanaendelea kuomba kama tendo la ibada ya Mkristo na kukataa kuchomwa kwa manukato na kuwatoa wanyama dhabihu katika mfumo ambao leo tunaishi chini ya sheria ya Kristo ambapo maombi yameagizwa na zingine siyo. Hivyo, pamoja na vyombo vya muziki katika ibada; Agano Jipya liko kimya. Hivyo nasi, tunatakiwa kukaa kimya.

Hatufanyi tohara kama agizo leo, kwa sababu tunapaswa kumsikiliza Kristo, siyo Musa. (Mat. 17:5). Vile vile, hatutumii vyombo vya muziki leo kwa sababu tunapaswa kumsikiliza Kristo, siyo Daudi.

***** Vyombo vya muziki zilitumika mbinguni; hivyo lazima zifae katika ibada ya Mkristo. "*Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wane na wale wazee ishirini na wane wakaanguka mbele za Mwana – Kondoo, kila mmoja wao anakinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.*" (Ufu. 5:8).

Jibu

Awali ya yote, Ufunuo ni kitabu kikuu chenye ishara na haipaswi kuchukuliwa kirahisi katika mambo yote. Kufuata fikra hii, tungepaswa kuwa na wanyama pamoja na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato (manukato), pamoja na filimbi (siyo kinanda au zeze) katika kanisa. Je, ye yote anaweza kuamini hivyo?

Pia, hakutakuwa na kuoa wala kuolewa mbinguni. (Mat. 22:30). Je tunaweza kuiondoa hapa? Hakutakuwa na ubatizo au meza ya Bwana mbinguni, lakini Kristo aliamuru yote yafanyike katika kanisa.

***** Inasemekana kwamba vyombo vya muziki zinakubalika katika miji, hivyo kwa nini isiwe katika kanisa?

Jibu

Kama mtu anweza kukaa kimya na kutafakari, anaweza kutaja mambo mengi ambayo yanakubalika kikamilifu nyumbani lakini hazifai katika ibada ya Mkristo katika kanisa. Kuosha mikono kama tendo la usafi, yafaa katika mji, lakini sio katika kanisa kama tendo la ibada. (Mk. 7:1-13). Kula nyama na mboga inakubalika nyumbani, lakini itakuwa haifai kuwekwa katika meza ya Bwana. Mji unaongozwa na sheria njema. Kitu chochote ambacho kinaongozwa kwa usahihi ni sahihi yote katika mji. Lakini katika kanisa lazima tufanye kile tu kilicho amuriwa katika Agano Jipya.

Kuna tendo linguine linalofanana na muziki wa kiroho katika kanisa ambalo Napenda kulishughulikia, hataivyo si sehemu ya somo letu la vyombo vya muziki. Hiyo ni kuunda kwaya ambayo inatumika katika huduma ya uimbaji. Tendo hili lote ni geni katika Agano Jipya. Ni geni pia kwa waalimu wa Agano Jipya kuhusiana na uimbaji katika kanisa.

Tumeamuriwa, "*Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;*" (Efe. 5:19). Kwa wale wanaopenda kwaya katika huduma zao, tunaweza kuwauliza, je mwengine anaweza kumtumikia Mungu badala yenu? Mwingine anaweza kuabudu badala yenu? Mwingine anaweza kula meza ya Bwana badala yenu? Kwa nini, basi, unataka mwingine akuimbie?

Ebu na tukazane katika kufuata maagizo ya Bwana katika yote tufanyayo.

Wenu katika Kristo,

J. D. Logan